

**MKATABA WA KUPANGISHA
NYUMBA**

BAINA YA

**HILARY CHRISPINE
(MWENYE NYUMBA)**

NA

**SURICATA SAFARIS LIMITED
(MPANGAJI)**

MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA ILIYOPO ENEO LA KIRANYI JIJI
LA ARUSHA MKOA WA ARUSHA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 1 January 2020

Kati ya

HILARY CHRISPINE, wa Arusha, mwenye simu namba 0763222293 (ambaye katika Mkataba huu anatajwa kama ni "MWENYE NYUMBA" katika mkataba huu kwa upande mmoja:

Na

SURIKATA SAFARIS LIMITED wa S.L.P 16301, Arusha, ambaye naye anatajwa kama ni "MPANGAJI" katika mkataba huu, kwa upande mwingine.

MAKUBALIANO YA KUPANGISHA NA KUPANGA NI KAMA IFUATAVYO:-

1. Mwenye nyumba amekubali kumpangisha "MPANGAJI" nyumba nzima kwa ajili ya ofisi katika nyumba yake iliyotajwa hapo juu katika mkataba huu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1/01/2020, hadi kuishia tarehe 31/12/2023 na baada ya kumalizika kwa kipindi hicho ikiwa mpangaji watapendelea kuongezea kipindi kingine cha upangaji huu naye mwenye nyumba asipokuwa na sababu za kuwakatalia utafanyika mkataba mwingine kufuatana na majadiliano na maafikiano ya wakati huo.
2. Kodi ya Upangaji huu ni **Shilingi Milioni Kumi na tatu (TShs.13,000,000/=)** (kwa mwaka mmoja, kodi ambayo italipwa mwanzoni mwa upangaji huu, naye mwenye nyumba kuiweka saini yake katika mkataba huu, kuthibitisha kupokea jumla ya **Tshs.13,000,000/=(Millioni kumi na tatu)** toka kwa mpangaji zikiwa ni kodi ya mwaka moja wa mwanzo.
3. Mpangaji haruhusiwi kuipangisha nyumba hiyo kwa mpangaji mwingine zaidi yake, wala haruhusiwi kuifanya aina yoyote ya marekebisho bila kupata idhini toka kwa mwenye nyumba kwanza.
4. Mpangaji watawajibika kujilipia matumizi yake ya umeme na maji kikamilifu bila ya kulimbikiza madeni na hii ni mbali na kodi ya upangaji huu.
5. Mpangaji atawajibika kuitunza nyumba hiyo katika hali ya usafi na siku ya kuhama watawajibika kuikabidhi nyumba hiyo ikiwa katika hali nzuri. Kwamba, endapo kitu chochote katika nyumba hiyo kukiharibika mpangaji watawajibika kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe ambazo haitamhusu mwenye nyumba.



Mwenye Nyumba





Mpangaji

6. Mpangaji wakiukatiza upangaji wake mwenyewe kabla ya kufikia mwisho wake, hawatakuwa na haki ya kumdai mwenye nyumba amfaidie kwa kipindi ambacho watakuwa amekwisha kukilipia na bado kutumika labda iwe ni mwenye nyumba ndiye aliyeukatiza.
7. Kwamba, mpangaji hawaruhusiwi kuingiza kitu chochote ndani ya nyumba hiyo ambacho kitahatarisha usalama wa nyumba pamoja na watu wengine kama moto (INFLAMABLE)
8. Mpangaji atawajibika kuomba kwa mwenye nyumba kipindi kingine cha upangaji huu miezi mitatu kabla ya mkataba huu kufika mwisho wake, naye endapo atakubaliwa atatakiwa kuwa tayari kulipia kipindi kingine mara tu kitakapoanza.
9. Kwamba, endapo patatokea kutoelewana baada ya kusaini Mkataba huu, basi upande utakaoathirika unaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya upande mwingine

Mkataba huu tumeandikiana hapa mjini Arusha tumeusoma, tumeuelewa na kuukubali ya kwamba ni sawa kwa kuziweka saini zetu tukiwa na akili timamu bila ya kulazimishwa wala kushawishiwa Leo tarehe 01 JANUARI 2020.

UMESAINIWA na KUWASILISHWA hapa Arusha
na **HILARY CHRISPINE**
Saini Mimi Mwenye Nyumba

SURICATA SAFARIS LIMITED
Saini upande wa Upangaji

DAVID TUHOYE
Shahidi wa Mwenye Nyumba

